



EO 2020-35: Sheria ya Utendaji kuhusu Kufunga Mwaka wa Masomo ya K-12 wa 2019-2020

Muhtasari:

- Tuko katika kipeo cha mgogoro wa afya ya umma. Afya, usalama, na ustawi wa wanafunzi wetu na walimu ndio kipaumbele chetu. Kanuni fulani za masomo ya K-12 hazina maana katika hali tuliyo nayo hivi sasa.
- Licha ya kipeo hiki, lazima elimu iendelee. Tuna wajibu wa kuwapa wanafunzi wetu nafasi za kujifunza wakati wa janga hili.
- Badala ya kufikiria juu ya kutii bila kukosa, tunahitaji kulenga maadili mengine – mawasiliano, busara, upendo, ubunifu, and ushirikiano.
- Kufundisha, kujifunza, na mtindo wa kuwasilisha masomo zitatofautiana kutoka wilaya moja hadi nyingine. Haiwezekani kutumia njia moja katika wilaya zote.
- Shule zitakapofunguliwa kwa mwaka wa masomo wa 2020-21, mabadikiliko ya ziada na huduma yatahitajika kwa wanafunzi. Kwa sasa, lazima tuhakikishe kuwa waliotarajiwa kufuzu wamefuzu na wale watakojiunga na vyuo wamefanya hivyo.

Vipengele muhimu vya Amri ya Utendaji (EO)

Kufungwa kwa shule/Siku na masaa/Mahudhurio/Kalenda

- **Kufungwa kwa mashule:** Vifaa vya mashule vimefungwa kwa muda wote uliobaki wa mwaka wa masomo, ila serikali iseme kuna usalama wa kufungua mashule tena na iondoe masharti. Kufungwa huku ni pamoja na michezo na shughuli zenye uhusiano na masomo.
- **Siku na masaa wakati shule zimefungwa kisheria:** Ruhusu siku 13 juu ya siku shule zimefungwa kisheria, zaidi ya siku 6 “za theluji.” Ruhusu siku 5 zaidi za mafunzo ya kikazi unapohesabu siku za kufundisha ili kusaidia walimu kujifahamisha na mtindo mpya wa kufundisha.
- **Mahudhurio:** Samehe asilimia sabini na tano (75%) ya kanuni ya mahudhurio tangu hali ya hatari ya jimbo ilipotangazwa.
- **Vifaa:** Amri ya Utendaji itaonyesha wazi kuwa vifaa vya wilaya vinaweza kutumiwa na wafanyakazi wa shule za umma na makontrakita kwa ajili ya kuwezesha masomo kwa njia ya tekinolojia, ila wasikaribiane (hakuna atayefanya kazi isiyo ya lazima

isipokuwa inayohitajika na wafanyakazi wakae umbali wa futi sita kutoka kwa mwingine).

- **Kalenda ya shule:** Ruhusu wilaya itumie kalenda iliyosawasishwa kwa mwaka wa masomo wa 2019-2020 na/au ianze mwaka wa masomo wa 2020-2021 kabla ya sikukuu ya wafanyakazi (yaani, Labor Day) bila kuhitaji ruhusa za ziada.

Kuendela na masomo na Mpango wa maamuzi kuhusu Ugonjwa wa Korona (COVID-19)

- **Mchakato wa kutuma maombi ya kuendelea na masomo:**
 - Ili kusamehe siku/masaa ya kiti ya ziada yanayohitajika, lazima wilaya ziwasilishe mpango wa kuendelea na masomo na mpango wa maamuzi yao kuhusu ugonjwa wa Korona (COVID-19).
 - Kuidhinishwa kwa maombi kutapitia hatua mbili: Kwanza, lazima ombi liangaliwe na kuidhinishwa na Wilaya husika (yaani, Intermediate School District, ISD) au mkuu wa shule za mkataba (charter school authorizer). Baada ya kuidhinishwa, ISD/mkuu wa shule za mkataba atawasilisha mipango hiyo kwa Idara ya Elimu ya Michigan (MI Department of Education, MDE) na “msamaha” kwa siku/saa zilizobaki utakubaliwa.
 - Lazima mpango uidhinishwe ili wilaya iendelee kupata msaada wa mwaka wa masomo wa 2019-2020 kutoka jimbo la Michigan.
- **Mpango wa kuendelea na masomo na vipengele vya maamuzi ya ugonjwa wa Korona (COVID-19):**
 - Maelezo jinsi wilaya itaendelea kutoa mafundisho, kwa njia yoyote ya ufundishaji.
 - Ahadi ya kuendelea kutoa chakula kwa wanaohitaji.
 - Ahadi ya kulipa wafanyakazi wote wa shule.
 - Ahadi ya kutoa huduma za afya ya kiakili.
 - Ahadi ya juhudi za kusaidia kutoa utunzaji wa watoto wa wafanyakazi wanaohitajika kazini.
- **Kumbukumbu muhimu:**
 - Ikiwa mpango utategemea kufundisha kupitia mtandao, wilaya ihakikishe kila mwanafunzi ana tekinolojia inayofaa yenye uwezo wa kuunganishwa kwenye mtandao.
 - Wanafunzi na wazazi wasiadhibiwe kwa kutoweza kushiriki kikamilifu katika mpango huo.
 - Wilaya zinaweza kushirikiana na nyingine au na mashirika ya nje ili watekeleze mipango yao.
 - Yanayofundishwa/ratiba za masomo ni maamuzi ambayo yanaafikiwa na maeneo yaliyo karibu na mashule.

Maagizo mengine

- **Kupima/Kuripoti:** Ondoa mitihani ya muhula wa machipuo. Ondoa mahitaji yote ya kisheria ambayo yanatumia data za kupima wanafunzi (A-F, Kusoma katika darasa la 3, kupimwa na walimu, malengo ya Mapatano ya Wilaya) kwa mwaka mmoja tu. Kwa

wanafunzi wanaotarajia kuingia mwaka wa mwisho wa masomo yao, ahirisha mtihani wa SAT mpaka muhula wa maanguko. Wakubalie wanafunzi wengine wa shule za sekondari kufanya mtihani wa PSAT muhula wa maanguko.

- **Mahafali ya Shule za Sekondari/Mtalaa wa Kustabili wa Michigan (Michigan Merit Curriculum):** Lazima wilaya zianzishe mpango/mchakato kutoa alama kwa wanafunzi wa mwaka wa mwisho, watoe alama zinazohitajika kufuzu, waidhinisha vyeti vya alama za wanafunzi, na kutunukia shahada. Wilaya zinahimizwa kutoa alama kwa mafundisho ya awali/uelewa wa yaliyomo na/au kutumia ufundishaji unaotegemea miradi, na potifolio/muhtasari wa yaliyotekelezwa, au tukio linalofanywa kwa muda fulani.
- **Eimu ya walemavu:** Lazima wilaya ziwasaidie wanafunzi na masomo yao yanayohitaji vifaa maalumu (Individualized Education Program, IEP) kwa kiwango kinachowezekana, lakini ieleweke wilaya zinapaswa kutoa huduma za kufidia wanafunzi walemavu wakati hali ya dharura itakapondolewa. Wilaya lazima zifuate maagizo yote ya Idara ya Elimu ya Marekani na Idara ya Elimu ya Michigan. Idara ya Elimu ya Michigan (MDE) imehimizwa kupata maagizo ya ziada na uwezo wa kubadilisha mambo kutoka Idara ya Elimu ya Marekani ambayo yanahusu wanafunzi wenye mipango ya kielimu ya wanafunzi binafsi (IEPs) na mipango ya 504 (yaani mipango ya kuwasaidia wanafunzi walemavu).
- **Kuthibitisha walimu na Kuendelea na masomo:** Inawapa wakaguzi wa elimu uwezo wa ziada wa kubadilisha mambo na kutoa shahada za kwanza za walimu na kuziidhinisha nyingine upya, ili kuzingatia viziwi vilivyosababishwa na ugonjwa wa Korona (COVID-19).
- **Mfumo wa kustaafu wa wafanyakazi wa shule za umma za Michigan (MPSERS):** Kufungwa kwa mashule hakutaathiri mchango au kiwango cha huduma katika MPSERS.
- **Mkataba wa wafanyakazi:** Amri hii ya Utendaji itekelezwe kwa njia ambayo iko sambamba na mkataba wa wafanyakazi.
- **Vifaa vya kulinda mtu binafsi (PPE) na vifaa vingine:** Inaruhusu na kuhimiza wilaya kusaidia mashirika yaliyoko katika jamii zao na vifaa vya PPE visivyotumika, vifaa vya usafi na vifaa vingine kama mashirika hayo yanavihitaji.